# MAANA YA: MASIKINI NA MJANE

2020 by Dennis Dickinson

"Masikini mtakuwa nao kila siku," Yesu akasema. Swali hapa ni je, nini maana ya masikini? Watu tofauti hutafsiri maana ya swala hili kwa njia mbalimbali. Kinacho jadiliwa hapa ni kwa wale wanao sema, "nitumie fedha ili nikutane na mahitaji ya masikini, mayatima na wajane."

Umasikini umekuwepo kwa miaka na mikaka na utakuwa daima. Maeneo ya kivita pengine hupuni visa vibaya vya mayatima na wajane. Vitani, hakuna maghala ya vyakula popote. Mazingira ya kijamii hufungwa kabisa wakati ambapo wengi hukumbana na makali ya njaa na kufa. Hii ndiyo maana halisi ya masikini.

Bibilia inapoelesea mambo haya, inaleta tofauti kamili ya umasikini kupindukia na kuwa na upungufu wa fedha. Kati ya masikini halisi na mjane halisi na wale ambao sio. Kati ya yule ambaye anafaa kuajibika kwa hao na yule mbaye hasitahili. Inatuonya pia kwa Timotheo wa kwanza 5 kuwa kanisa likitumia rasilimali zake kwa wale ambao hawasitahili, basi, halitakuwa na rasilimali kwa wale ambao wanafaa.

Kiheburania, neno mjane humaanisha yule ambaye ametengwa, ameachwa na kutubwa. Kwa Gikiriki, neno mjane humaanisha kuwa na pengo ama mwanya. Umbali na utupu. Mbali na chochote kinachowesekana kupata kile anacho kiitaji maishani. Mbali na uwezekano wa kupata mahitaji yake itakayo muwezesha kuishi. Hivyo basi maandiko kwa Timotheo wa kwanza 5 inasema, "Si wajane wote ni wajane halisi," kutupilia mbali maana au tafsiri ya ulimwengu. Kingeresa kinawesa sababisha iwe vigumu kuona haya. Mlango huo huo unasema yeye si mjane halisi ikiwa ako na wale ambao wanasitahili na wako na uweso wa kumushughulikia; kutacha tu, watoto wake waliokomaa, wajukuu wake waliokomaa na watu wa jamii na jamaa wake wa karibu. Kwenywe kitabu cha Ruthu mjane alilindwa na mke wa kijana yake alieaga. Pia Timotheo wa kwanza 5 kinasema wanawake wanastaili kulinda wajane wao ili Kanisa lisiwe na msiko. Inafaa na kwa hakika ni wajibu wa jamii kushughulikia swala hili. Ni hapa ndio wajane na mayatima wanafaa, kwanza kuwa na jamii. Kanisa na viongozi wake wanaonywa wasiingilie na kuchukua nafasi ya jamii.

Vile vile mayatima ambao hawana wazazi ama jamaa wa karibu kuwachukua na kukaa nao wako tofauti na kuwa tu masikini. Hapa pia kuna haja ya ufafanusi. Kihebrania neno masikini, ina maana ya, kuhusunika na kuinama chini kwa unyenyekevu. Hii ni kujibu wengine huku kichwa kuinamishwa jini kwa sababu ya aibu. Gikiriki neno hufafanua muombaji ambaye hana kitu hata kidogo. Yule ambaye hukaa kando ya barabara kuomba huruma huku akistahimili makali ya njaa. Yesu alipeana kwa watu sambuli hii, lakini si kwa wengine.

Najua makao ya watoto yatima ambapo baadhi ya watoto waliomo si yatima. Pia nafaamu barabara kwamba wakiniomba pesa ya watoto yatima masikini, wanaousika hawasemi hilo kwa uaminifui kwangu. Hawaniambii hilo kwa ukweli. Niliambia mtu mmoja kama huyo anayesimamia makao ya watoto yatima kwamba atume watoto hao nyumbani kwa wazazi wao na jamii zao badala kushinda akiomba pesa kwa niapa yao. Huduma nyingi siku hizi wamekua wa kuomba omba wanaotarajia kulibwa kutoka kwa wanaume na wake kwa kisingisio ni za mayatima na wajane. Picha wanazokuonyesha ni za makusanyiko ya watu huku wakipeana vitu mbali mbali kwa

yeyote kila upande. Watoto wako n a nyumbani kwao na wajane wako na familia zao na hakuna yeyote anafaa kupeana jojote kwa mtu yeyote. Kuomba omba kwa kila mtu ulimwenguni kwa jina la wakristo ili watumiwe pesa zaidi kulisha miji yote injini mwao, ni swala Bibilia inasema watu wa Mungu hawastaili kuunga mkono. Kuna viongozi wengi wa Kanisa ambao hawajawai enda kwa Bibilia kujifaamisha na kile inavyofunza.

Viongozi halisi wa kanisa wanafaamu kuwepo kwa wajane halisi wanaoitaji kwa hakika usaidisi mara kwa mara. Wajane ambao hawana watu wa jamaa zao walio hai, ambao hawawezi kufanya kazi hata kidogo, ambao wanawesa kufa njaa ikiwa hawasaidiwa na mtu. Hawa ndio Wajane halisi ambao Bibilia inaongea juu yake.

Wakristo lazima wapate mtazamo wa mafundisho ya Bibilia, sio tu kwa neno au kifungu kilijoondolewa kutoka lengo hitajika kutumika kujipatia pesa, na si kutumia rasilimali za hapo awali visivyo. Rasilimali ambazo Mungu kapeana kwa ajili ya wale walio na mahitaji makubwa miongoni mwetu. Asili ya kibinadamu, ikiwa vile ilivyo kujukulia fursa  ya wengine. Lazima kuitikia, kwa hitaji ikiwa linafaa kwa wajane halisi, mayatima halisi na masikini halisi. Wengine wanasitahili kwenda kwa jamii zao, jamaa, majirani na marafiki; na ikihitajika serikali za mitaa na serikali kuu wakati tuko na baa la njaa kuu kwa halaiki. Swala la muhimu mukubwa linalojitokesa ni kua tayari kutubu kuhusu haya yote na kumutazamia na kutekemea Mola anaye kutana na mahitaji ya watu wote kupitia kwa njia mbalimbali, Serikali kuu, mamulaka za mitaa, Makanisa, Marafki, Majirani, na familia; Kumushukuru kwa kukutana na mahitaji na kumtazamia awese kutufunza neno lake tusitumie alijotupa visivyo.

## BIBILIA Na UMISHONARI

Huwa napokea maombi mara kwa mara kuusu Bibilia na ninekua nikijibu watu hivi, “Enda ukasome haya maandiko hadi uyafaamu ndani ya moyo wako na uyatii na **shida yako kuusu Bibilia itafika tamati…”**

Wakolosayo 4:16 Na barua hii ikisha somwa kati yenu, isomwe pia kwa kanisa la Leodesia; Na muhakikishe kwamba mumesoma ile itokayo Leodesia.

Wathesolonike wa kwanza 5:27 Nawaweka jini ya kiapo mbele za Bwana kwamba barua hii itasomwa kwa wapendwa wote.

Mara nyingi nimesoma vitabu viote via Bibilia kwa watu na wanapenda sana.

2020 by Dennis Dickinson
whitestonemissions
(Haya maandishi yawesa kupeanwa bure ilimradi hayauswi)

# Maana ya: Masikini na Mjane

# Na

# Bibilia na Umishonari